# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
# CHUO CHA UALIMU MONDULI

S.L.P 5, **MONDULI**.
Simu: +255 (0)27 2538026
Fax +255 (0)27 2538060

Web: www.mondulitc.ac.tz
Email: <mondulitc@gmail.com>

---

**Kumb. Na: MON/TC/GF15/164** **03/02/2022**

**Bw. Kibwana A. Mlinda**

**YAH: KUSHINDA KAZI YA UFUNDI UASHI NA BOMBA**

Ndugu husika na mada tajwa hapo juu.

Napenda kukupa taarifa kuwa, kutokana na tendo la usahili lililofanyika katika Chuo cha Ualimu Monduli tarehe **29/01/2022**, lililoendeshwa na kamati ya Ujenzi ya Chuo, ulishinda kazi ya Ufundi UASHI NA BOMBA.

Aidha kamati inakupongeza kwa ushindi huo na inakushauri kufanya kazi kwa mujibu wa Makubaliano/ Mkataba ili kuongeza ufanisi katika kazi yako.
Hivyo utapigiwa simu muda wowote kuanzia sasa kwa ajili ya kujaza mkataba na kuanza kazi.

Mwisho tunakutakia kazi njema.

Wako katika Ujenzi wa Taifa.

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU MONDULI
S.L.P. 5 MONDULI

..............................
Prof.Samwel M. Irira
**MKUU WA CHUO**

# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# FOMU YA MKATABA WA UJENZI KWA FUNDI CHUO CHA UALIMU MONDULI

## A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA

| | | |
|---|---|---|
| 1 | MWAJIRI | Mkuu wa Chuo<br>Chuo cha Ualimu Monduli<br>S. L. P. 5, MONDULI<br>Kny:<br>Katibu Mkuu<br>Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia |
| 2 | JINA NA ANWANI YA FUNDI (*Mwajiriwa*) | Jina: KIBWANA ALLY MLINDA<br>Anwani: S. L. P 3 MONDULI<br>Simu: 0764877878 |
| 3 | ENEO LA UJENZI | ***Monduli teacher's college*** |
| 4 | MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI | KUJENGA BOMA NA KAZI ZOTE ZA BOMBA |
| 5 | GHARAMA YA UFUNDI (*Including Skills Development Levy*): | ~~16,400,000/=~~<br>17,900,000/= |
| 6 | MUDA WA MKATABA (Tangu Kusainiwa kwa Mkataba): | Tarehe ya Kusaini 29.01.2022<br>Muda: MIEZI 5 (MITANO)<br>Tarehe ya Kuanza Kazi ……………<br>Tarehe ya Kumaliza Kazi …………… |
| 7 | MASHARTI YA MALIPO: | • Hakuna Malipo ya Awali<br>• Fundi atalipwa baada ya kazi husika kukamilika na kukaguliwa |

**B: MASHARTI YA JUMLA MKATABA**

1. Mwajiri atatoa vifaa vyote vya ujenzi kulingana na maelekezo ya Mtaalamu Mshauri. Zaidi ya hayo mwajiri atatoa maji na umeme.

2. Mwajiri atatoa vitendea kazi kama karai na chepe.

3. Fundi atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi *(kama inavyooneshwa katika kiambatanisho cha malipo kwenye mkataba huu.)* na mwongozo wa Mtaalamu Mshauri, kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.

4. Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kulipa hasara zote zilitokana na uzembe au makusudi.

5. Fundi atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kiujenzi.

6. Fundi kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.

7. Fundi atahusika na vitendo *(kama wizi, uharibifu wa mali za chuo)* vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.

8. Fundi kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.

9. Kiasi cha asilimia 5% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa Miezi Mitatu baada ya kazi kukamilika *(Retention Money)* na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufanyika.

10. Kiasi cha 4.5% kitatolewa kwenye gharama ya malipo yako kama *Skills Development Levy*,SDL.

11. Ucheleweshaji wa Kazi:

- Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo.

12. Ucheleweshaji wa Vifaa na Malipo:

- Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri *(kutokana na fedha au vifaa)*, Fundi ataongezewa muda wa kumalizia kazi.

13. Uvunjwaji wa Mkataba:

- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya Chuo.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Fundi wake hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya Mtaalamu Mshauri.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au kidarua atajihusisha na mahuisiano ya kimapenzi na mwana chuo.

**14.** Maelekezo ya kazi yatatolewa na msimamizi mkuu wa kazi (Clerk of works) na mwajiriwa (Fundi) ataomba malipo fedha kwa kazi aliyoifanya kwa mkuu wa Chuo kupitia msimamizi wa kazi na atalipwa endapo ukubwa wa kazi aliyofanya itakaguliwa na kufika angalau 30%.

**MWAJIRI:**

Saini: ……………………………

Jina : Prof. Samwel Ima

Cheo: Mkuu wa Chuo

CHUO CHA UALIMU MONDULI S.L.P. 3 MONDULI

Tarehe: 29.01.2022

**FUNDI:**

Saini: ……………………

Jina: KIBWANA A. MLINDA

Cheo: FUNDI

Tarehe: 29/01/2022

**SHAHIDI WA MWAJIRI**

Saini: ……………………………

Jina: LAMON M. MTWEVE

Cheo: K/M/MKUU WA CHUO

Tarehe: 29/01/2022

**SHAHIDI WA FUNDI**

Saini: Nsoerga

Jina: Mahad i mwoarga

Cheo: Fundi

Tarehe: 29/1/2022

| MUAINISHO WA GHARAMA ZA KAZI ZA UASHI<br>JENGO JIPYA LA BWENI (NEW DORMITORY) | | |
|---|---|---|
| S/N | KAZI<br>JENGO JIPYA LA BWENI | GHARAMA |
| 01. | Kusafisha eneo kwa kuondoa udongo wenye mboji | 500,000 |
| 02. | Kuchimba msingi kimo kisichozidi 750cm | 1,000,000 |
| 03. | Kuweka zege kwenye msingi | 1,000,000 |
| 04. | Kujenga ukuta wa msingi wenye unene 230mm | 1,700,000 |
| 05. | Kupanga mawe,blinding na kuweka DPM | 1,000,000 |
| 06. | Kumwaga jamvi C. 20 (100mm oversite concrete), kuweka sakafu ya rough na kumwagilizia siku saba (7) | 2,000,000 |
| 07. | Kujenga ukuta wenye unene 150mm | 1,500,000 |
| 08. | Kufunga formwork kwenye ring beam | 500,000 |
| 09. | Kuweka chuma kwenye ring beam | 200,000 |
| 10 | Kumwaga zege kwenye ring beam na kumwgilizia siku saba (7) | 500,000 |
| 11. | Kujenga kozi tatu za tofali juu ya ring beam pamoja na kupandishwa gebo | 500,000 |
| 12. | Kuweka frem za madirisha na milango | 450,000 |
| 13. | Kupiga plasta ndani na nje ya jengo | 3,000,000 |
| 14. | Kuweka vigae kwenye sakafu ya bweni,vyoo na kuta zake | 2,200,000 |
| 15. | Kuziba matundulizu baada ya kupauwa | 200,000 |
| 16. | Kuchimbia bomba za umeme ukutani. | 150,000 |
| 17. | Kujenga incinerator kwa maelekezo ya mshauri elekezi | 500,000 |
| 18. | Kufanya kazi zote za bomba (plumbing) | 700,000 |
| 19. | Kuchimba mashimo ya chemba za maji taka pamoja na kujengea . | 300,000 |
| | JUMLA | ~~16,400,000/=~~<br>17,900,000/= |

N.B: Kazi zingine ndogondogo zitakazojitokeza, utazifanya bila kuathiri gharama.

Jina la mwombaji (FUNDI) KIBWANA ALLY MHINDA Saini [signature]

Namba ya Simu ya mwombaji (FUNDI) 0764877878

Tarehe 29/01/2022 27-01-2022